# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NNE

**03 SEPTEMBA, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 03 SEPTEMBA, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 *[The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 *[The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021].*

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**40. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Stendi katika Mji wa Chemba ambao unakuwa kwa kasi.

**41. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano ya ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Bunda.

**42. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilichukua eneo la Mlima Nkongore ambao ndani yake kulikuwa na makazi ya Wananchi na kuliwekea *bicon* na

kusababisha Kaya zaidi ya 10 zilizochukuliwa maeneo yao kuishi kwa hofu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzilipa fidia Kaya hizo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**43. MHESHIMIWA HASSAN SADIKI SIMAI (NUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio kuimarisha miundombinu ya Miradi ya Maji ya *African Adaptation Programme (AAP)* iliyojengwa kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi ili kuondokana na mahitaji makubwa ya maji dhidi ya ongezeko la watu katika Jimbo la Nungwi.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**44. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inatumia mikakati gani kudhibiti mapato yatokanayo na gawio kutoka kwenye Kampuni ambazo Serikali inamiliki Hisa chini ya asilimia 50.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**45. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa Wanafunzi wote kunufaika na mikopo kwa asilimia 100 bila kujali shule walizosoma;

(b) Je, Serikali inawasaidiaje Wazazi waliostaafu ambao wameshindwa kuchangia gharama za Elimu ya Juu.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**46. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini ujenzi wa Kiwanda cha Vifaa Tiba vinavyotokana na zao la Pamba Dutwa Mkoani

Simiyu utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu ulishafanyika.

**47. MHESHIMIWA JULIANA DIDAS MASABURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Kiwanda cha *MUTEX* kilichopo Musoma Mjini kinafunguliwa na kurudisha ajira kwa Vijana wa Mkoa wa Mara.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**48. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wa kulisaidia na kulijengea uwezo Jeshi la Kujenga Uchumi la Zanzibar (JKU).

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 49. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ilishawahi kulifanyia matengenezo muhimu gari lililotolewa na Mbunge kutoka kwa Wafadhili toka Japan na kupelekwa Kituo cha Polisi cha Gonja katika Jimbo la Same Mashariki Mwaka 2015.

### 50. MHESHIMIWA ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA (MTONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifungua Kituo cha Polisi cha Betrasi kilichopo katika Jimbo la Mtoni Zanzibar ambacho kimefungwa kwa zaidi ya mwaka sasa.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

### 51. MHESHIMIWA SHANIF JAMAL MANSOOR (KWIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Hungumalwa – Ngudu hadi Magu kwa kiwango cha lami.

## WIZARA YA NISHATI:

### 52. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Umeme Wilayani Tunduru chenye uwezo wa kupokea 132 KV ambazo ni uhitaji halisi kwa Wilaya za Tunduru, Nanyumbu na Masasi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**53. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itaondoa Wanyama wakali hasa Tembo katika Tarafa ya Mlali na kuwarudisha kwenye Hifadhi ya Mikumi kwa kuwa wamekuwa kero kwa Wananchi.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***[Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu]***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021 *[The Accountants and Auditors (Registration) (Amendments) Bill, 2021].*

**DODOMA**
**03 SEPTEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**